



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

HALMASHAURI YA WILAYA YA KIBONDO



Unapojibu tafadhali taja:

Kumb.HW/A/S.50/22/VOL.II/149

Tarehe: 27. 04. 2023

YAH: MABADILIKO YA TANGAZO LA KAZI

Halmashauri ya Wilaya ya Kibondo ilitangaza nafasi za kazi kupitia tangazo **Kumb. Na. H/W/A/S.50/22/VOL.II/131** la tarehe **04/04/2023** na **HW/A/S.50/22/134** la tarehe **18/04/2023**,

Ofisi imepokea maelekezo kutoka kwa Katibu, Ofisi ya Rais Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi Umma kwa barua yenye **Kumb Na.AB.161/259/01/D/12** ya tarehe 20/04/2023 kutumia kanzidata ya wasailiwa waliofaulu usaili kwenye saili za nafasi za kazi zilizopita lakini hawakupata nafasi kutokana na nafasi zilizokuwepo wakati huo kuwa chache.

Kwa msingi huo, nafasi za kazi za Mtendaji wa Kijiji Daraja III zilizotangazwa usaili hautafanyika na badala yake tutatumia Kanzidata.

Kwa upande wa nafasi tatu (03) za Madereva Daraja II na Msaidizi wa Kumbukumbu Daraja Ia II, Halmashauri haina Kanzidata (Database), tangazo la nafasi hizo litaendelea na baada ya uchambuzi kukamilika wasailiwa wenye sifa wataitwa kwa ajili ya usaili.

Naomba Radhi kwa Usumbufu Utakaojitokeza.

Rutema D.M
MKURUGENZI MTENDAJI (W)
KIBONDO

